HOTUBA YA NAIBU WAZIRI WA MADINI MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA (MB.) WAKATI WA KUFUNGUA JUKWAA LA USHIRIKISHWAJI WA WATANZANIA KATIKA SEKTA YA MADINI KATIKA UKUMBI WA AICC JIJINI ARUSHA TAREHE 16 MACHI - 2023.

Mhe. John V. Mongella, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Arusha,

Ndg. Zelothe Steven, Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa

Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa,

Mhe. Felician Mtahengerwa, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha,

Dkt. AbdulRahman Mwanga,Kamishna wa Madini,

Prof. Idris Kikula,Mwenyekiti wa Tume ya Madini,

Makamishna wa Tume ya Madini,

Kamati ya Ushirikishwaji wa Watanzania,

Mha. Ramadhan Lwamo, Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini,

Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini (Tume ya Madini, TGC,GST, TEIT, STAMICO),

Mhe. Mrisho Gambo, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Arusha,

Maafisa Madini Wakazi -Arusha, Kilimanjaro, Mirerani na Manyara na Tanga,

Viongozi wa Dini mliopo,

Wadhamini wetu Wakuu Kampuni za Twiga Minerals

Corporation Limited, Transec Tanzania Limited, Max Steel Limited na Apex Holdings (A) Limited na CMS Tanzania Limited,

Wadhamini wetu wote,

Watumishi wa Wizara ya Madini, Tume ya Madini na Taasisi za Wizara ya Madini,

Kampuni za uchimbaji wa madini na Wachimbaji wa Madini,

Watoa huduma na washiriki wote wa Jukwaa la Pili la Utekelezaji wa Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini,

Wenyeviti wa vyama vya Wachimbaji Taifa, Mkoa na Wilaya,

Wachimbaji na Wafanyabiashara ya Madini,

Wageni Waalikwa,

Ndugu wanahabari,

Mabibi na Mabwana,

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…….

Ndugu Washiriki, Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii aliyotupatia kuwepo hapa leo katika ufunguzi wa jukwaa la Pili la Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini. Jukwaa hili lina Kauli mbiu "***Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini kwa kufungamanisha na Sekta Nyingine kwa uchumi imara wa Nchi***". Ni azma ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuona Sekta ya Madini inachangia ipasavyo katika Pato la Taifa na inachochea sekta nyingine za uchumi katika kuleta maendeleo.

Ndugu washiriki, Kati ya Malengo Makuu ya Sera ya Madini ya Mwaka 2009 ni kufungamanisha Sekta ya Madini na Sekta Nyingine za Uchumi. Katika kutekeleza hili Serikali pamoja na mambo mengine inatakiwa: kuandaa na kusimamia utekelezaji

wa programu ili kuongeza ushirikiano wa Sekta ya Madini na sekta nyingine za uchumi; kuyataka makampuni ya madini kununua bidhaa na huduma ndani ya nchi; na kuwasaidia Watanzania ili waweze kusambaza bidhaa na huduma zenye ubora kwa Kampuni za madini.

Ndugu washiriki, Serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ya Madini Sura 123 mwaka 2017. Pamoja na mambo mengine suala la Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini lilipewa kipaumbele ili kuakikisha Kampuni zote za Madini katika shughuli zote zinazohusisha mnyororo mzima wa uzalishaji na biashara ya Madini wanatoa kipaumbele kwa Watanzania. Mabadiliko hayo ya Sheria, yalipelekea kutungwa kwa Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania za Mwaka 2018 ili kuweka usimamizi thabiti katika utekelezaji wa masuala yote ya Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini nchini.

Ndugu washiriki: Usimamizi wa utekelezaji wa Ushirikishwaji wa Watanzania umepelekea kuibua na kuchochea ongezeko la fursa mbalimbali katika nafasi za ajira na mafunzo, uhawilishwaji wa teknolojia, utafiti na maendeleo, matumizi ya huduma na bidhaa zinazotolewa na kuzalishwa na Watanzania. Suala hili limesababisha Sekta ya Madini kuwa na mchango mkubwa nchini katika kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuwa fursa nyingi

zinatolewa kwa watanzania na kuwapa nafasi ya kukuwa kiuchumi na kiteknolojia. Aidha, matumizi ya huduma na bidhaa zinazozalishwa nchini na zile zinazotolewa na watanzania yamepelekea kuongezeka kwa mapato ya Serikali kupitia malipo ya kodi na tozo mbalimbali katika utoaji wa huduma na bidhaa husika.

Ndugu Washiriki, Baada ya kuanzishwa kwa Tume ya Madini iliyopewa pia majukumu ya kusimamia masuala ya Ushirikishwaji wa watanzania katika Sekta ya madini, kumekuwa na mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali kwa uchache kama ifuatavyo:

Ajira na Mafunzo: Ajira kwa Watanzania katika migodi mikubwa zimeongezeka kutoka 6,668 mwaka 2018 hadi kufikia 15,341 mwaka 2022. Aidha katika nafasi zinazohitaji kupata uzoefu kutokana na kukuwa kwa teknolojia duniani, kumekuwa na utaratibu wa Kisheria wa urithishwaji watanzania kwa nafasi zinazoshikiliwa na wageni. Hii ni kutimiza azma ya Serikali ya kuongeza idadi kubwa ya Watanzania wanaoshikilia nafasi za uongozi katika makampuni ya uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini.

Pia, kumekuwa na mafanikio makubwa kwa watanzania wanaopata mafunzo mbalimbali ya kujengewa uwezo wa kufanya

kazi ambazo baadhi zilikuwa zinafanywa na wageni. Kwa mwaka 2022, jumla ya watanzania 8,066 walipatiwa mafunzo mbalimbali katika Sekta ya Madini na kujengewa uwezo katika utendaji kazi ambapo jumla ya fedha Shilingi **bilioni 3.4** zilitumika.

Ndugu Washiriki, Wizara kupitia Tume ya Madini imeendelea kusimamia **Manunuzi ya bidhaa na huduma** kwa kuhakikisha kipaumbele kinatolewa kwa watanzania kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura ya 123. Usimamizi huo umekuwa na matokeo chanya kwa kuongeza idadi watanzania wanaotoa huduma na kuuza bidhaa kuanzia migodi ya uchimbaji mdogo, ya kati hadi ya uchimbaji mkubwa wa madini nchini.

Katika mwaka 2022 jumla ya Dola za Kimarekani **bilioni 2.22** sawa na **asilimia 97.4** ya manunuzi yote ya kampuni za madini yalifanyika kwa kutumia kampuni za Watanzania, ukilinganisha na Dola za kimarekani **milioni 238.71** sawa na **asilimia 46** ya manunuzi yote kwa mwaka 2018. Pia, kumekuwa na ongezeko la watoa huduma ambapo kwa mwaka 2022 wamefikia 1386 sawa na **asilimia 81** ikilinganishwa na mwaka 2018 ambapo kulikuwa na watoa huduma 623.

Ndugu Washiriki, uelewa wa masuala ya Ushirikishwaji wa Watanzania umeongezeka kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2022. Elimu inayoendelea kutolewa imesaidia

Watanzania wengi kuona fursa mbalimbali katika sekta ya madini. Vilevile kampuni za kigeni zimeendelea kuwasilisha mipango ya Ushirikishwaji wa Watanzania na uundaji wa Kampuni za ubia na Kampuni za Kitanzania. Mpaka sasa **kampuni 1,319** zimepitishiwa mipango yao na Tume ya Madini. Nitoe rai kwa Kampuni zote kuendelea kutimiza matakwa ya Sheria ya Madini Sura ya 123 kuhusuiana na suala la ushirikishwaji wenyeji.

Ndugu Washiriki, Wizara pia imeendelea kusimamia Uhawilishwaji wa teknolojia (*Technology Transfer*) na Utafiti na maendeleo (*Research and Development*) kulingana na matakwa ya Sheria. Katika kipindi cha Mwaka 2018 hadi Mwaka 2022, Uhawilishwaji wa teknolojia umeendelea kufanyika katika kuboresha matumizi ya mitambo yenye uwezo mkubwa katika uzalishaji na kuongeza tija kwa kiasi kikubwa. Pia, watanzania wameendelea kujengewa uwezo kufanya kazi mbalimbali kwa kutumia teknolojia ambazo hapo awali hazikuwepo nchini.

Ndugu Washiriki, pamoja na mafanikio makubwa yaliyotokea katika utekelezaji wa Ushirikishwaji wa Watanzania, kumekuwa na changamoto mbalimbali ambazo tukizifanyia kazi zitapelekea Ushirikishwaji wa Watanzania kuongezeka na kuleta manufaa zaidi kwa Watanzania. Changamoto hizo ni pamoja na:

Baadhi ya kampuni za kigeni kutokuwa tayari kufanya ubia na kampuni za kitanzania na hivyo kutokidhi matakwa ya Sheria ya Madini. Hii imepelekea kukosa sifa na kushindwa kuidhinishiwa mikataba ya kutoa huduma na bidhaa migodini kwa sasa.

Changamoto nyingine ni **Upungufu wa viwanda vikubwa nchini kwa ajili ya uzalishaji wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya uchimbaji na uchenjuaji wa Madini**. Mitambo na vipuri kwa ajili ya uchimbaji na uchenjuaji havizalishwi kwa wingi nchini, hivyo vinapohitajika migodini huagizwa kutoka nchi za nje kutoka kwa wazalishaji halisi wa mitambo na vipuri (*Original Equipment Manufacturers* - OEM).

Ndugu Washiriki, pia kumekuwa na changamoto ya **Wamiliki wa leseni na Watoa huduma kutotekeleza ipasavyo wajibu wao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni.** Masuala ambayo yamekuwa hayazingatiwi kwa kiasi kikubwa katika kutimiza matakwa ya ushirikishwaji wa Watanzania ni pamoja na kushindwa kuwasilisha mpango na taarifa za utekelezaji wa ushirikishwaji wa Watanzania kila Mwaka, kutokufuatwa taratibu za manunuzi, na kuingia mikataba kwa kutotangaza zabuni husika Nchini na kutoidhinishwa na Tume ya Madini. Suala hili limepelekea Watanzania kukosa fursa mbalimbali katika Sekta ya

Madini. Niwatake wamiliki wa leseni na watoa huduma kutekeleza wajibu wao kikamilifu.

Ndugu Washiriki na Viongozi, kuna changamoto pia katika **Uelewa mdogo wa masuala ya Ushirikishwaji wa Watanzania** miongoni mwa Watanzania na wawekezaji. Hii imesababisha baadhi ya Watanzania na Kampuni za Kitanzania kushindwa kutimiza matakwa ya Sheria na kuweza kushiriki katika fursa zilizopo katika Sekta ya Madini.

Vilevile suala la baadhi ya Watanzania na Kampuni za Kitanzania **kushindwa kutoa huduma katika viwango na ubora** uliokubaliwa katika mikataba waliyoingia imekuwa ni changamoto katika kutekeleza dhana ya ushirikishwaji watanzania. Hii, inasababisha Kampuni za madini kuingia gharama za ziada za kupata bidhaa na huduma zenye ubora na hivyo kampuni za kitanzania kukosa zabuni wakati mwingine. Nitoe rai kwa migodi kuendelea kutoa elimu kwa watoa huduma na wasambazaji wa bidhaa ili kuendelea kuboresha huduma na bidhaa zao.

Ndugu Washiriki, baadhi ya watoa huduma na wasambazaji wa bidhaa **huweka bei kubwa za bidhaa na huduma** katika zabuni ukilinganisha na bei halisi ya soko. Hii pia ni changamoto inayosababisha watanzania wengi kupoteza fursa ya kusambaza bidhaa na huduma migodini. Naomba kuwa kumbusha

watanzania wenzangu kuwa dhana ya kuwa kampuni za madini zina fedha na zinaweza kununua kwa bei yoyote huduma na bidhaa zetu sio kweli. Tujitahidi kuwa na uhalisia ili tupate fursa hizi.

Ndugu Washiriki, Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini imeandaa jukwaa hili mahsusi kwa ajili ya: kuonesha fursa mbalimbali zilizopo katika sekta ya madini; kuwajengea uwezo wasambazaji na watoa huduma; kusikiliza changamoto zilizopo katika utekelezaji wa dhana ya ushiriki wa watanzania; na kutatua changamoto zilizopo kwa manufaa ya nchi yetu. Pia nimeambiwa kuna baadhi ya kampuni zitapata muda wa kuongea na watoa huduma na wasambazaji wa bidhaa. Niwaombe watanzania wenzangu kuchangamkia fursa hizo kwa kujua mahitaji ya kampuni hizo

Ndugu Washiriki, kabla sijahitimisha hotuba hii naomba niwakumbushe kuwa, Tanzania ni mwanachama wa Asasi ya Kimataifa ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia **(The Extractive Industries Transparency Initiative** (EITI). Taasisi ya TEITI ni moja ya taasisi zilizochini ya Wizara ya Madini yenye jukumu la msingi la kuhakiki mapato yatokanayo na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia na kuangalia fedha zilizozilipwa kwa serikali na kampuni na

kulinganisha fedha zilizopokelewa na kuziweka wazi kwa wananchi wote kupitia ripoti.

Aidha, TEITI inajukumu la kuhakikisha kampuni zinazofanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia zinaweka wazi kwa umma taarifa za shughuli zao kulingana na Sheria ya TEITA ya Mwaka 2015. Nitoe rai kwa makapuni yote yatoe ushirikiano kwa TEIT na wananchi wasome ripoti za TEIT.

Mwisho nichukue fursa hii kuwakumbusha kuwa Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini itaendelea na usimamizi thabiti kuhakikisha kuwa, kipaumbele kinatolewa kwa bidhaa zinazozalishwa nchini na bidhaa na huduma zinazotolewa na Watanzania.

Ndugu washiriki, Baada ya kusema hayo natamka rasmi kuwa jukwaa la pilli la utekelezaji wa Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini **limefunguliwa rasmi.**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Asanteni sana kwa kuunisikiliza.